

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

*Simu:* 255-262961500/1  
*Nukushi:* 255-262961502  
*Barua pepe :* [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
*Tovuti :* [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



*OFISI YA RAIS,*  
*IKULU,*  
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*  
*CHAMWINO,*  
*S.L.P 1102,*  
*40400 DODOMA.*

*Lusaka*  
*24 Oktoba, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais Samia Suluhu Hassan amesema katika utekelezaji wa kuwapa wananchi kipaumbele katika maendeleo ameamua kutenga hekta 20 za ardhi katika Bandari Kavu eneo la Kwala mkoani Pwani.

Rais Samia ameyasema hayo ikiwa ni zawadi kwa wananchi wa Zambia wakati akihutubia katika maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa nchi hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu.

Aidha, Rais Samia amesema wakiongelea mgawanyo wa raslimali, msisitizo ni kila mwananchi kunufaika huku akiongeza kuwa yeye pamoja na Rais Hakainde Hichilema ni waumini wa kuwawezesha wananchi katika maendeleo ya Kiuchumi.

Kaulimbiu ya *'Kuchapusha Maendeleo ya Kitaifa kupitia Ugawwanaji wa Raslimali'* amesema Rais Samia imekuja wakati muafaka si tu kwa Zambia lakini pia kwa nchi nyingine za Afrika ikiwemo Tanzania.

Rais Samia amesema siku ya Uhuru unaosherehekewa leo ni kwasababu waasisi wa Mataifa hayo mawili waliamini, wakapambania walichoamini na kuandaa mipango ya utekelezaji.

Wakati huo huo nchi hizo mbili zimedhamiria kujenga bomba jipya la gesi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia, pia wamepanga kuimarisha bomba la mafuta TAZAMA pamoja na reli ya TAZARA.

Rais Samia anaendelea na ziara ya siku 3 Jamhuri ya Zambia kwa mwaliko wa Rais Hichilema ikiwa na malengo ya kuimarisha uhusiano wa kindugu pamoja na kiuchumi.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

